



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA AFYA**  
**HOSPITALI YA BENJAMIN MKAPA**



**TAARIFA KWA UMMA**  
**Februari 6, 2023, Dodoma**

**BMH KUOKOA MAISHA YA WATOTO WENYE MATATIZO YA MOYO NCHINI**

Hospitali ya Benjamin Mkapa, leo Februari 06, 2023 imesaini makubaliano ya ushirikiano wa kutoa Huduma za Upasuaji wa Moyo kwa Watoto na Shirika lisilo la Kiserikali la Childrens Heart Charity Association la Nchini Kuwait.

Akizungumza kuhusu mkataba wa makubaliano hayo mbele ya waandishi wa Habari Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo Dkt. Alphonse B. Chandika amesema makubaliano hayo yameangazia maeneo makuu matatu.

Eneo la kwanza ni la Msaada wa kibinadamu ambapo Hospitali ya Benjamin Mkapa na Shirika la Childrens Heart Charity Association watagharamia matibabu ya Moyo kwa Watoto wenye matatizo yanayohitaji upasuaji.

Eneo la pili ni Kuhakikisha vifaa tiba vinavyohitajika kuwezesha matibabu ya Moyo kwa Watoto vinapatikana kusaidia huduma hizo kuwa endelevu.

Eneo la tatu ni kuwajengea uwezo madaktari, wauguzi na wataalamu wa huduma za uchunguzi na matibabu ya Magonjwa ya Moyo wa Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuwawezesha kuendelea kutoa huduma hizo kwa ufanisi na weledi hasa matumizi ya teknolojia mpya.

Utiwaji Saini wa Makubaliano hayo umeshuhudiwa na Mheshimiwa Balozi Hemed Mgaza Mkurugenzi Idara ya Mashariki ya Kati, Mheshimiwa Saidi Shaib Mussa, Balozi wa Tanzania Nchini Kuwait, Mheshimiwa.....Balozi wa Kuwait nchini Tanzania.

Pamoja na utiwaji Saini wa mkataba wa Makubaliano hayo tayari timu ya Madaktari, Wauguzi na Wataalamu wa Huduma za matibabu ya Moyo kutoka Kuwait wamefika katika Hospitali ya Benjamin Mkapa kutoa huduma za Uchunguzi na Matibu ya Moyo kuanzia Feburuari 3 na watakuwepo hadi Feburuari 9, na inatarajiwa kuwa zaidi ya Watoto 100 watafanyiwa uchunguzi na kupata matibabu ya upasuaji wa Moyo.

